**HOTUBA YA MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI (MB) WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA) KWENYE UFUNGUZI WA TOVUTI KUU YA HUDUMA KWA WATUMISHI WA UMMA(WATUMISHI PORTAL) KATIKA UKUMBI WA HAZINA–DODOMA, TAREHE10, FEBRUARI, 2017.**

**Wahesimiwa Mawaziri;**
**Dkt. Laurean Ndumbaro, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora);**
**Makatibu Wakuu Mliopo;**
**Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora);**
**Wawakilishi wa Vyama vya Wafanyakazi Mliopo;**
**Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na Watumishi wa Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora);**
**Ndugu Watumishi wa Umma Mliopo hapa;**
**Waandishi wa Habari;**
**Wageni Waalikwa;**
**Mabibi na Mabwana,**
**Habarini za Leo!**

Awali ya yote, nianze kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwa wote mliokubali kuitikia wito wa kushiriki nasi katika uzinduzi wa Tovuti Kuu ya Huduma kwa Watumishi wa Umma (WATUMISHI PORTAL). Pili napenda nichukue fursa hii kukupongeza wewe Katibu Mkuu (Utumishi) pamoja na Menejimenti ya Ofisi yetu kwa kufanikisha utengenezwaji wa Tovuti hii ninayoizindua leo. Tovuti hii dhumuni lake ni kutoa huduma kwa Watumishi wa Umma kwa Njia ya Mtandao.

1. **Ndugu Watumishi wa Umma;**

   Kama alivyoeleza Katibu Mkuu, tarehe 23 Juni ya kila mwaka, ni siku maalum iliyotengwa na Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika, kuadhimisha siku ya Kimataifa ya Utumishi wa Umma. Maadhimisho ya siku ya Utumishi wa Umma yalikubaliwa kwa madhumuni ya kutambua mchango wa Watumishi wa Umma katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

   Tangu sherehe hizo zilipoanzishwa hapa Tanzania Mwaka 2002, zilikuwa zikiadhimishwa kwa njia ya maonesho ya huduma zinazotolewa na Taasisi mbalimbali za Umma.

Hata hivyo sherehe za Mwaka jana ziliadhimishwa kwa njia tofauti, ambapo kila Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Umma, alielekezwa kuzungumza na Watumishi wake ili kubaini changamoto zinazowakabili katika Utendaji wa Majukumu yao ya kila siku.

**2. Ndugu Watumishi wa Umma;**

Mimi binafsi nilitembelea Mikoa na Wilaya mbalimbali ikiwemo hapa Dodoma ambapo nilikutana na kujionea changamoto ambazo Watumishi wa Umma wanakabiliana nazo. Zipo changamoto ambazo nilizipatia majibu na kutoa maelekezo pale pale na naamini kuwa baadhi ya Watumishi wa Umma walifanikiwa kutatua kero zao. Niliahidi kuwa changamoto nyingine za muda mrefu zinazohitaji mabadiliko ya kisera na kimifumo, tutaendelea kuzifanyia kazi.

**3. Waheshimiwa Mawaziri, Makatibu Wakuu na Watumishi wa Umma;**

Moja ya changamoto niliyoibaini katika ziara hizo ilikuwa ni kuendelea na mifumo ya kizamani ambayo kwa kiasi kikubwa, inatokana na kuendelea kutumia mawasiliano ya barua, ambazo wakati mwingine huchukuwa muda mrefu kumfikia mhusika, au kutomfikia kabisa.

Ni dhahiri kuwa changamoto hii haikubaliki katika zama hizi za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano **(ICT),** na ninafurahi kwamba Wataalam wetu wameweza kuitafutia ufumbuzi kwa kubuni na kutengeneza Tovuti maalum ya Watumishi (**Watumishi Portal**) ambayo tunashuhudia uzinduzi wake leo. Hongerani sana.

**4. Waheshimiwa Mawaziri, Makatibu Wakuu na Watumishi wa Umma mliopo;**

Tovuti hii inayotoa Huduma kwa Watumishi wa Umma kwa njia ya mtandao, ni mahsusi kukabiliana na baadhi ya changamoto zinazowakabili Watumishi wa Umma.

Matumizi ya Tovuti yatasogeza huduma karibu zaidi na Watumishi wa Umma na hivyo kupunguza muda wa kushughulikia malalamiko na pia gharama za kusafiri nje ya kituo cha kazi ili kupata huduma na mrejesho wa haki na stahiki za Watumishi wa Umma.

**5. Ndugu Watumishi wa Umma;**

Ninyi ndiyo Injini ya Serikali na chachu ya kuleta maendeleo kwa Wananchi. Kwa sababu hiyo, Ofisi yangu imebuni na kusanifu Tovuti hii Kuu ya Huduma kwa Watumishi wa Umma. Kama nilivyokwishaeleza hapo juu lengo la Tovuti hii ni kuwarahisishia

Watumishi wa Umma kupata huduma na mrejesho mbalimbali kwa njia rahisi na ya haraka popote walipo na muda wowote. Kwa kufanya hivyo, tutawaongeza morali kwao kufanya kazi na hatimaye kuongeza tija katika kuwahudumia Wananchi.

6. **Ndugu Watumishi wa Umma,Wana Habari, Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana;** Tovuti nitakayoizindua leo, imetengenezwa ili kutoa huduma tatu za Kiutumishi; Huduma ya Kwanza ni ya kushughulikia malalamiko ya Watumishi wa Umma. Huduma hii ina lengo la kuwasaidia Watumishi wa Umma kufikisha haraka malalamiko yao kwa Mamlaka za juu pale yanaposhindikana na kusikilizwa au kutatuliwa na Waajiri wao wa karibu. Mbali ya huduma hii kuwarahisisishia Watumishi wa Umma kufikisha malalamiko yao kwa haraka, itawawezesha pia kuyafuatilia kirahisi na kujua kila hatua iliyofikiwa kuhusiana na ushughulikiaji wa lalamiko lililowasilishwa na kupatiwa ufumbuzi kwa njia ya kielektroniki. Kama nilivyoeleza hapo awali, huduma hii haitamlazimu Mtumishi wa Umma kusafiri au kuwa nje ya kituo cha kazi;

7. **Ndugu Watumishi wa Umma;** Huduma ya Pili ni ile ya kuwawezesha Watumishi wa Umma wanaotaka kuhama/kubadilishana vituo vya kazi kuweza kubadilishana taarifa za awali. Huduma hii imelenga kuwaunganisha kwa njia ya mtandao Watumishi wa Umma wanaotaka kubadilishana vituo vya kazi. Tofauti na iliyo sasa ambapo Watumishi wa Umma wanatumia mbao za matangazo katika Taasisi, vyumba vya mashine za kutoa fedha (ATM), n.k na wamekuwa hawana uhakika wa taarifa hizo kuwafikia Watumishi wa Umma walengwa. Lakini sasa kwa kutumia Tovuti hii ya Watumishi Portal, Watumishi wataweza kubadilishana taarifa na kisha kuziarifu Mamlaka husika kwamba nafasi ya kuhama imepatikana. Kwa kutumia njia hii ya Tovuti, Watumishi wataweza kubadilishana taarifa hizo kwa uharaka, uhakika na kupata wigo mpana zaidi wa ubadilishanaji wa vituo vyao vya kazi.

8. **Ndugu Watumishi wa Umma;** Pamoja na ubora wa njia hii, napenda ieleweke kuwa baada ya Watumishi wa Umma kukubaliana na kuafikiana nia yao kubadilishana vituo vyao vya kazi, itawapasa kufuata taratibu za kawaida za Kiutumishi ili kukamilisha mchakato wa uhamisho.

   Haitegemewi kwamba baada ya Watumishi wenyewe kukubaliana watahama bila kupitia kwa Waajiri wao. Hatua hii ni ya kuiwezesha Serikali kuwa na kumbukumbu za wapi walipo Watumishi wake.

9. **Ndugu Watumishi wa Umma;** Huduma ya Tatu inahusu kupata Taarifa binafsi zinazomhusu Mtumishi wa Umma kuhusiana na mabadiliko yanayotokea kwenye Taarifa zake za Kiutumishi na Mshahara. Huduma hii itamwezesha Mtumishi kufahamu mabadiliko ya Taarifa zake za Kiutumishi na Mishahara yaliyokwishafanywa na kuwekwa kwenye mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara **(HCMIS**) na Mwajiri wake. Kwa mfano, Mtumishi wa Umma ataweza kupata taarifa za matukio yake ya kiutumishi na mishahara kama yameingizwa kwenye mfumo au bado; au yamehakikiwa; na kama matukio hayo yamekubaliwa au kukataliwa n.k. Pia Mtumishi wa Umma ataweza kupata taarifa kuhusiana na mshahara wake kwa mwezi husika. Kwa ujumla ni mabadiliko ya taarifa za Kiutumishi.

10. **Ndugu Watumishi wa Umma;**
Huduma hii itaongeza uwazi na uwajibikaji kwa Maafisa Utumishi, Waajiri na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika kushughulikia masuala mbalimbali ya Kiutumishi na mishahara kwa Watumishi wa Umma. Nimekuwa nikipokea malalamiko kadhaa kuhusu Watumishi kuzungushwa na Waajiri wao kuhusu mabadiliko ya taarifa zao za kiutumishi. Hali hii inajidhihirisha pale ambapo nimekuwa nikiambiwa katika ziara zangu za kikazi jinsi Watumishi wa Umma wanavyonyimwa taarifa sahihi zinazohusu matatizo yao. Ni imani yangu kuwa huduma hii itakuwa jibu kwa Watumishi waliokuwa wakizungushwa na kupata majibu yasiyo sahihi.

11. **Ndugu Watumishi wa Umma**;
Huduma hii pia itaongeza usahihi wa Taarifa zilizopo katika Mfumo wetu wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara kwa kuwa Mtumishi mwenyewe atakuwa na uwezo wa kujua usahihi wa Taarifa zake zilizopo kwenye Mfumo.
Aidha, Huduma hii itampatia Mtumishi wa Umma taarifa za mwisho za malipo yake ya Mshahara ikiwa ni pamoja na Makato (jambo ambalo tunategemea litaongeza uwazi kwa Watumishi wa Umma kuhusu usahihi wa malipo na makato waliyonayo kwenye mshahara yao. Hata pale anapochelewa kupata hati ya malipo ya mshahara (***Pay Slip***), kupitia tovuti hii ataweza kuziona taarifa hizo bila kuchelewa.

12. **Ndugu Watumishi wa Umma;**
Huduma hizi ni mwendelezo wa hatua za kuufanya Utumishi wa Umma kuwa wa kisasa. Napenda kuwaarifu kuwa huduma nyingine nyingi zitaongezwa kwenye Tovuti hii kwa

kadiri tutakavyoona inafaa kwa kuzingatia maoni ya Wadau wote na changamoto zilizopo na zitakazoendelea kujitokeza. Kupitia Tovuti hii, tutafurahi kupata mrejesho na mapendkezo mengine kwa kadri mtakavyoona inahitajika ili tuweze kuuboresha.

13. **Ndugu Watumishi wa Umma,Wana Habari, Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana;**
Napenda kutumia fursa hii kuwaasa na kuwahamasisha Watumishi wa Umma kuzitumia huduma hizi kwa ukamilifu ili kuwarahisishia ufuatiliaji wa haki zao na kuongeza ufanisi kwa Waajiri wenu. Endapo Watumishi wa Umma wataona taarifa zao zimekosewa, basi watatakiwa kuwataarifu Waajiri wao wakiwa na vielelezo vya kuthibitisha usahihi wa taarifa hizo ili Waajiri nao waweze kuzirekebisha mara moja ikiwa ni pamoja na kufanya marekebisho ya taarifa hizo kwenye Mfumo Shirikishi wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara. Kwa upande wa Waajiri, napenda kuwaasa kufanya kazi na kusimamia maslahi ya Watumsihi wenu kwa weledi na kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali inayotolewa na Serikali kuhusu Usimamizi wa Watumishi wa Umma.

14. **Ndugu Watumishi wa Umma;**
Mtaona kwamba Serikali yenu ya Awamu ya Tano ina malengo maalum ya kuwajengea mazingira mazuri ya kazi. Wakati Serikali inaendelea kuwekeza katika mifumo ya kurahisisha Utendaji wenu wa Kazi, ni dhahiri kuwa na ninyi mnao wajibu kwa Serikali na Wananchi ambao ndio walipa kodi zinazotuwezesha kujenga mifumo hii na kulipia maslahi na haki zenu. Kama ambavyo nimekuwa nikisisitiza siku zote, wapo baadhi ya Watumishi wa Umma wanafanya kazi bila kuzingatia umuhimu wa tija na ufanisi katika kutoa huduma za Serikali na hivyo kuathiri utendaji na utoaji wetu wa huduma kwa Umma.

Kama nilivyoeleza hapo awali Watumishi wa Umma wanayo nafasi muhimu katika jamii kwa kuwa ndiyo injini ya kuleta maendeleo ya haraka. Kutokana na hali hiyo, Serikali inafanya jitihada za makusudi kuboresha mifumo ya kiutendaji na mifumo ya utoaji wa huduma kwa Umma ili kupunguza matumizi ya uendeshaji wa Serikali na kuongeza tija na ufanisi.

**15. Ndugu Watumishi wa Umma;**

Napenda kuwakikishia kuwa Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kuboresha mifumo ya kiutendaji na mifumo ya utoaji wa huduma kwa lengo la kuongeza ufanisi na kupunguza gharama za uendeshaji wa Serikali kwa njia mbalimbali ikiwamo matumizi ya TEHAMA kupitia dhana ya Serikali Mtandao.

Kwa kuwa Watumishi wa Umma ndio Injini na chachu ya kuleta maendeleo kwa wananchi, Ofisi yangu itaendelea kubuni mifumo bora ya utoaji huduma kwa Wananchi, na pia kubuni njia mbalimbali za kuwarahisisishia Watumishi wa Umma kupata huduma kwa njia rahisi na ya haraka popote walipo na muda wowote. Ni imani yangu kuwa kuwarahisisishia Watumishi wa Umma kupata huduma kwa urahisi na haraka, kutawaongezea morali ya kufanya kazi na hatimaye kuongeza tija katika kuwahudumia Wananchi.

**16. Ndugu Watumishi wa Umma na Wageni Waalikwa;**

Nafahamu mmesubiri muda mrefu kuona na kushuhudia mapinduzi ya kutoa huduma kwenu. Naomba sasa mniruhusu kuzindua rasmi Tovuti Kuu ya Huduma kwa Watumishi wa Umma.

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA.**